# Ofisi ya Udhibiti wa Magonjwa ya Kuambukiza

# Miongozo ya Ugawaji wa Chanjo ya NH COVID-19 kwa Awamu ya 1a
## Tarehe 5 Februari 2021

(mabadiliko katika rangi **nyekundu**)

NH inachukua mtazamo wa awamu wa uzinduzi wa chanjo, ikilenga idadi kubwa ya watu na mgawo wa awali wa chanjo kutoka kwa watengenezaji. Watu hawa muhimu watapokea chanjo katika Awamu ya 1a. Awamu zinazofuata zimeainishwa kwenye hati tofauti, Mpango wa Chanjo wa NH COVID-19. Madhumuni ya hati hii ni kusaidia kufanya uamuzi kuhusu idadi ya watu wa Awamu ya 1a. Mwongozo kuhusu awamu za baadaye utatolewa kama inavyopatikana. Hati hii ni badilifu, na inaweza kubadilika, kwani ufanisi wa chanjo na data usalama zinaendelea kujitokeza na mwongozo wa kitaifa unaendelea kubadilika. Hati hii inatoa:

- Muhtasari wa idadi tatu za watu ndani ya awamu ya 1a
- Maelezo ya kina ya watu katika mpango wa ugawaji wa awamu ya 1a wa New Hampshire
- Kanuni za waajiri na wengine wanaohusika kwa ugawaji wa chanjo palipo upatikanaji mdogo wa dozi

## Awamu ya 1a: Upatikanaji Mdogo wa Dozi, "Awamu ya Kuanza"

Kitengo cha New Hampshire cha Huduma za Afya ya Umma (DPHS) kinajumuisha vikundi vifuatavyo vya chanjo chini ya Awamu ya 1a: 1) wahudumu wa afya walio katika hatari katika vikundi hatari zaidi na vya wastani; 2) watu wazima wazee katika mipangilio ya utunzaji wa makazi; na, 3) waitikiaji wa kwanza. Mchoro ufuatao ni muhtasari wa Awamu ya 1a wa Ugawaji wa Chanjo ya NH, na maelezo ya ziada ya vikundi hapa chini:

### Wahudumu wa Afya Walio Katika Hatari

**Hatari kubwa:**Wahudumu wa afya kwenye mstari wa mbele wanaotoa huduma ya moja kwa moja na wafanyakazi wasaidizi wenye hatari ya kuambukizwa na vioevu vya mwili au erosoli.

**Hatari ya wastani**: Wafanyakazi wasiokaribiana moja kwa moja au wanaokaribiana kwa muda mfupi na mgonjwa.

### Wazee Katika Mipangilio ya Utunzaji wa Makazi

Wakazi wa vituo vya utunzaji wa muda mrefu (LTCF), uuguzi wenye ujuzi (SNF), na vituo vya kuishi kwa kusaidiwa (ALF).

### Waitikiaji wa Kwanza

**Moto na EMS:** Wafanyakazi wote wa kibinafsi, wa umma na wa kujitolea wa huduma za matibabu na dharura.

**Utekelezaji wa Sheria:** Maafisa wote waliothibitishwa au kuapishwa wa kutekeleza sheria katika NH, iwe wameajiriwa kwa kudumu au kwa muda.* Inajumuisha utekelezaji wa sheria ya Shirikisho ambayo haijajumuishwa kwenye mgao wa shirikisho.

**Waitikiaji wa COVID-19**: Wafanyakazi walio na mwitikio wa NH COVID na mawasiliano ya mgonjwa au virusi vya SARS-CoV-2, ikiwemo wanamaabara wanaopima COVID-19 na wafanyakazi wa ukusanyaji wa violezo.

*Haijumuishi maafisa wanaofanya kazi katika vituo vya marekebisho, ambayo yamejumuishwa katika awamu ya baadaye.

## Maelezo ya Idadi ya Watu Ndani ya Awamu ya 1a

### I. Wahudumu wa Afya Walio Katika Hatari

New HampshireDHHS inajumuisha katika Awamu ya 1a ya mkakati wa mgawo wa chanjo wahudumu wa afya ambao:

(1) Wanafanya kazi katika hali ambapo hatari ya usambazaji wa SARS-CoV-2 ni kubwa, au

(2) Wako katika hatari kubwa ya kuambukiza maambukizo kwa wagonjwa walio katika hatari kubwa ya kifo na ugonjwa mbaya.

Sambamba na Taaluma za Kitaifa za Sayansi, Uhandisi, na Tiba (NASEM), NH inafafanua wahudumu wa afya walio katika hatari kuwa wahudumu **wanaolipwa au wasiolipwa** ambao ni **matabibu na wafanyakazi wengine** wanaowatunza wagonjwa katika **mazingira anuwai** ikiwa ni pamoja na: hospitali za papo hapo, urekebishaji na magonjwa ya kiakili; kliniki za wagonjwa wa kutembea na huduma za haraka; vituo vya dialisisi; vituo vya kuchangia damu, viungo, na tishu; nyumba za uuguzi, na mipangilio mingine (angalia Jedwali la 1). Kikundi hiki kitajumuisha majukumu ya jadi ya huduma ya afya lakini pia kinaweza kujumuisha wengine ambao wamepata mafunzo rasmi ya matibabu ambayo huwawezesha kufanya taratibu za utunzaji wa kliniki. Kwa mfano, wataalamu wa masomo ya shule wasiokuwa na leseni hawajumuishwi mara kwa mara katika ufafanuzi huu wa wafanyakazi wa afya isipokuwa ikiwa wamepata mafunzo kama haya. Mtu huyo hahitaji kupata shahada ya kliniki, lakini anatarajiwa kuwa anakaribiana kwa wagonjwa wakati wa kazi yake, pamoja na wale wanaosambaza au kupeana chanjo ya COVID-19 kama wafamasia; wafanyakazi wa plasma na wachangiaji damu, wauguzi wa afya ya umma; wanamaabara wa COVID-19; na wasimamizi wa mazishi, wahudumu wa vyumba vya kuhifadhia maiti na wataalamu wengine wa huduma ya kifo.

**Jedwali la 1: Mipangilio ambapo wahudumu wa afya wa Awamu ya 1a hufanya kazi**

| Mpangilio | Majukumu[1] |
|---|---|
| ***Hospitali za papo hapo, urekebishaji na magonjwa ya kiakili*** | Nyingi |
| ***Nyumba za uuguzi, vituo vya kuishi kwa kusaidiwa*** | Nyingi |
| ***Mipangilio ya huduma ya wagonjwa wa kutembea*** | |
| Kliniki za wagonjwa wa kutembea na huduma za haraka | Nyingi |
| Vituo vya dialisisi; vituo vya kuchangia damu, viungo, na tishu | Nyingi |
| ***Mipangilio mingine*** | |
| Shule za K-12 | Muuguzi wa shule |
| Huduma ya afya ya nyumbani | Msaidizi wa afya ya nyumbani, msaidizi wa huduma binafsi, tabibu wa mambo ya kazi |
| Huduma za mazishi | Mtu anayetia dawa kwenye maiti, msimamizi wa mazishi, mkurugenzi wa mazishi, meneja |
| Maduka ya rejareja | Mfamasia, fundi wa maduka ya dawa |

| | |
|---|---|
| Vituo vya marekebisho | Daktari, muuguzi |
| Makao ya jimbo yaCOVID-19 | Wafanyakazi, mtoaji wa usafiri |
| Nyumba za kikundi kwa watu wanaopona ambapo walioambukizwa COVID-19 wanakaa | Muuguzi, wafanyakazi wengine wa matibabu |
| Nyumba za kikundi kwa watu wenye magonjwa mengi yenye hatari | Muuguzi, wafanyakazi wengine wa matibabu |

[1]Hii sio orodha kamili ya majukumu ambayo yanafaa kwa chanjo ya Awamu ya 1a katika mipangilio hii. Jukumu la kazi litaamua watu wanaostahiki kama wahudumu wa afya wa Awamu ya 1a walio katika hatari.

Kwa kutarajia kuwa usambazaji wa chanjo utakuwa mdogo sana, DPHS imewapanga wahudumu wa afya walio katika hatari kwenye vikundi vitatu vidogo vya hatari kubwa, wastani na hatari ndogo kabisa. Kategoria za hatari zaidi na za wastani pekee zimejumuishwa katika Awamu ya 1a:

**i. Hatari kubwa**–iliyojumuishwa katika Awamu ya 1a: Wafanyakazi wa kliniki wa mstari wa mbele ambao hutoa huduma ya moja kwa moja kwa wagonjwa na wafanyakazi wasaidizi walio katika hatari ya kuambukizwa na maji ya mwili au erosoli (kwa mfano, ED, ICU, huduma ya haraka, matabibu wa kupumua, dawa ya kazi, wafanyakazi wa upimaji wa COVID-19 , wafanyakazi wa huduma za mazingira, usalama, n.k.)

**ii. Hatari ya wastani**–iliyojumuishwa katika Awamu ya 1a: Wafanyakazi wasiokaribiana moja kwa moja au wanakaribiana kwa muda mfupi na mgonjwa (kwa mfano, PT/OT, wafanyakazi wanaopeleka chakula, makasisi, makarani wa kitengo, wachunguzi wa kuingia wa COVID-19, wakalimani wa ana kwa ana, usajili wa wagonjwa, watumishi wa maegesho ya hospitali, watoa chanjo, nk.)

**iii. Hatari ndogo**–iliyojumuishwa baada ya Awamu ya 1a: Wafanyakazi wa utawala na wengine wasiokaribiana na wagonjwakwa hali inayotarajiwa ya mara kwa mara (kwa mfano rekodi za matibabu, usimamizi wa hospitali, malipo, wafanyakazi wa jikoni ambao hawapeleki chakula, maabara yasiyo ya COVID-19, n.k.) Wafanyakazi hawa ni muhimu kwa kudumisha miundombinu ya afya. Wafanyakazi hawa watapewa chanjo mapema iwezekanavyo mara baada ya Awamu ya 1a kukamilika.

Jedwali la 2 hapa chini linaonyesha kategoria za kazi ndani ya hospitali au mipangilio ya utunzaji wa wagonjwa wa kutembea ambayo inaweza kufikia ufafanuzi wa mhudumu wa afya aliye katika hatari, pamoja na mifano ya kazi maalumu na kiwango chao cha hatari. Sababu ya njia hii ya ziada kuainisha wahudumu wa afya walio katika hatari ni kupunguza uhusiano na uainishaji wa kawaida wa Rasilimali Watu. Orodha kamili ya kazi ndani ya kila kikundi katika mipangilio hii inapatikana katika Kiambatisho cha A. Matabaka ya hatari yanajumuishwa kama mwongozo, lakini yanategemea muktadha na mpangilio wa kazi (kwa mfano, madaktari ambao hufanya kazi ya simu pekee wanapaswa kuzingatiwa kama "wenye hatari ndogo"). Kwa usaidizi zaidi wa kufanya maamuzi ya kuwachanja wahudumu wa afya walio katika hatari, zingatia Kiambatisho cha B.

**Jedwali la 2: Kategoria za kazi, mifano na viwango vya hatari**

| Kategoria | Mifano ya Kazi | Kiwango cha Hatari Kilichopendekezwa |
|---|---|---|
| **Wafanyakazi wa kliniki wa mstari wa mbele**<br>*Wanaokaribiana na wagonjwa moja kwa moja* | Daktari, muuguzi, msaidizi wa daktari, mfanyakazi wa huduma ya nyumbani | Kubwa |

| | | |
|---|---|---|
| **Wafanyakazi wa mstari wa mbele wasio wa kliniki**<br>*Wanaokaribiana na wagonjwa moja kwa moja* | Wanamaabara wa COVID-19, walinzi, wasafishaji wa jengo | Kubwa |
| **Wengine wa kliniki**<br>*Wanaokaribiana kwa kiasi fulani na wagonjwa moja kwa moja* | Matabibu wa mambo ya kazi, wanasaikolojia, mafundi wa uchunguzi, wafanyakazi wa jamii | Wastani |
| **Chakula/Rejareja**<br>*Wanaokaribiana kwa kiasi fulani na wagonjwa moja kwa moja* | Wafanyakazi wanaopeleka chakula, wafamasia wa rejareja | Wastani |
| **Chakula/Rejareja**<br>*Wasiokaribiana na wagonjwa moja kwa moja* | Wapishi, keshia, wafanyakazi wanaoandaa chakula, waosha vyombo | Ndogo |
| **Wengine wasio wa kliniki**<br>*Wasiokaribiana na wagonjwa* | Wafanyakazi wa matengenezo, wanasayansi wa kibiolojia, watumaji | Ndogo |
| **Huduma za utawala, ukarani na kifedha**<br>*Wasiokaribiana na wagonjwa* | Meneja wa rasilimali watu, karani wa malipo, mchambuzi wa bajeti | Ndogo |
| **Kompyuta/Teknolojia ya Habari**<br>*Wasiokaribiana na wagonjwa* | Wataalamu wa usaidizi wa kompyuta, msimamizi wa hifadhidata, mfanyakazi wa kuingiza data | Ndogo |

## II. Wazee Katika Mipangilio ya Utunzaji wa Makazi

NH inajumuisha watu wazima wazima walio wazee katika mazingira ya makazi katika Awamu ya 1a kwa sababu ya athari kubwa ya COVID-19 katika mipangilio ya utunzaji wa makazi ya watu wazima katika NH. Idadi hii inajumuisha vikundi viwili:

1) Wakazi wa kituo cha utunzaji wa muda mrefu (LTCF) na uuguzi wenye ujuzi (SNF)
2) Wakazi wa kituo cha kuishi kwa kusaidiwa (ALF)

Wafanyakazi katika mipangilio hii wanazingatiwa kama wahudumu wa afya walio katika hatari hapo juu na pia watapokea chanjo katika Awamu ya 1a. Watu wazima wazee wanaoishi katika vituo vya kuishi vya kujitegemea, hata wale walio katika hali sawa na LTCF, watapewa chanjo baada ya 1a kwa sababu makazi yao hayana mikusanyiko na hayajapata athari kubwa katika NH.

## III. Waitikiaji wa Kwanza

Waitikiaji wa kwanza wamefafanuliwa kama ifuatavyo:

- **Huduma za matibabu ya moto na dharura (EMS):** Wafanyakazi wote wa kibinafsi, wa umma, na wa kujitolea na EMS ambao kazi yao inawaweka katika hatari kubwa ya kuambukizwa COVID-19
- **Utekelezaji wa sheria:** Maafisa wote waliothibitishwa au kuapishwa wa utekelezaji wa sheria katika NH, iwe wameajiriwa wa kudumu au wa muda ambao jukumu laolinahusisha kukaribiana mara kwa mara na umma. Hii ni pamoja na wafanyakazi wa Utekelezaji wa Sheria wa Shirikisho wanaofanya kazi katika NH ambao hawatapewa chanjo kupitia mipango ya shirikisho. Hii haijumuishi maafisa wanaofanya kazi katika vituo vya marekebisho, ambao wamejumuishwa katika awamu ya

baadaye.Hii pia haijumuishi wafanyakazi wa usalama katika maeneo yasiyokuwa ya kliniki (kwa mfano, vituo vya rejareja, taasisi za masomo).

Kwa kutarajia kuwa usambazaji wa chanjo ya kwanza utakuwa mdogo sana, DPHS imegawa zaidi waitikiaji wa kwanza walio hatarini katika vikundi vitatu vya hatari kubwa, wastani na ndogo. Kategoria za hatari kubwa na wastani pekee zimejumuishwa katika Awamu ya 1a:

I. **Hatari kubwa**– waitikiaji wa kwanza waliojumuishwa katika Awamu ya 1a ni wale ambao wanatarajiwa kwa sababu ya jukumu lao la kitaalamu la kukaribiana moja kwa moja na wagonjwa.
II. **Hatari ya wastani** – waitikiaji wa kwanza waliojumuishwa katika Awamu ya 1a ni wale ambao wanatarajiwa kwa sababu ya jukumu lao la kitaalamu la kutokaribiana moja kwa moja na wagonjwa. Waitikiaji hawa wa kwanza hutoa msaada kwa watoa huduma wa moja kwa moja wa wagonjwa/utunzaji.
III. **Hatari ndogo** – walioojumuishwa baada ya Awamu ya 1a: waitikiaji wa kwanza waliosalia. Wafanyakazi hawa ni muhimu katika kudumisha miundombinu ya utendaji. Wafanyakazi hawa watapewa chanjo mapema iwezekanavyo mara moja Awamu ya 1a itakapokamilika.

**Waitikiaji wa NH COVID-19:**Watu wanaoshiriki katika uitikiaji wa jangakatika mashirika anuwai ya umma na ya kibinafsi ambao wako katika hatari kubwa ya kuambukizwa COVID-19 kutokana na jukumu lao maalumu. Hii ni pamoja na watoa chanjo, vitengo vya upimaji, wakusanyaji waviolezo, wafanyakazi wa afya ya umma wanaokaribiana na wagonjwa wa COVID-19 na watu wao wa karibu, na wafanyakazi wa maabara ya COVID-19.

## Kipaumbele cha Watu katikaAwamu ya 1a

Kwanza, toa chanjo kwa wahudumu wa afya na waitikiaji wa kwanza walio katika hatari ambao wanastahili kuwa "wenye hatari kubwa zaidi" kabla ya"wenye hatari ya wastani." Tena, utabakaji wa hatari unategemea sana jukumu na mpangilio wa kazi.

Kisha wape kipaumbele wafanyakazi kulingana na hatari za kikazi na za kibinafsi. Kategoria zilizoonyeshwa hapa chini hazijaorodheshwa katika mpangilio wa kipaumbele, lakini zinapendekeza uzingatiaji wa vipaumbele ndani ya awamu ya 1a. Hizi ni pamoja na lakini sio tu wafanyakazi ambao:

- Wana hali ya hatari za matibabu (ambao wanachagua kufichua)
- Wana zaidi ya umri wa miaka 65
- Wanafanya kazi kwa vitengo vya COVID-19
- Wanatoa huduma ya mgonjwa ya moja kwa moja
- Wanaopaswa kufanya kazi bila PPE za kutosha
- Wameathiriwa kwa kiasi kikubwa na COVID-19 kama vile watu katika vikundi vidogo vya kimbari na kikabila
- Wale waliokuwa na COVID-19 iliyothibitishwa katika siku 90 zilizopita.

## KIAMBATISHO CHA A: Kazi Maalum za Wafanyakazi Ndani ya Mipangilio ya Huduma ya Afya

Jedwali hili ni toleo lililopanuliwa la Jedwali la 2 hapo juu. Jedwali hili linajumuisha kategoria za wafanyakazi katika mipangilio ya huduma ya afya na kazi maalum ndani ya kategoria hizi. Madhumuni ya jedwali hili ni kusaidia wapangaji wa chanjo katika kuamua ni nani anayestahili kupata chanjo na katika awamu gani. Kumbuka orodha hii haijumuishi kila kazi ambayo inaweza kuwapo katika mpangilio wa huduma ya afya, lakini inatolewa kama mwongozo.

**Jedwali la Kiambatisho cha A: Kazi kulingana na Kategoria**

| Kategoria na Utabakaji wa Hatari wa NH | Kazi – Sio kwa Mpangilio wa Alfatebi |
|---|---|
| **Wafanyakazi wa Kliniki wa Mstari wa Mbele**– Wanaokaribiana na wagonjwa moja kwa moja wako katika **hatari kubwa**. Wale ambao hufanya kazi kwa umbali au hawakaribianina wagonjwa moja kwa moja hawapaswi kujumuishwa kama walio katika hatari kubwa. | Wakufunzi wa Riadha |
| | Madaktari wa meno na matabibu wengine wa afya ya kinywa |
| | Wahudumu wa Afya ya Meno na Wasaidizi |
| | Wataalamu wa Msaada wa Moja kwa Moja |
| | Waitikiaji wa Matibabu ya Dharura, Mafundi na Wahudumu wa Hali za Dharura |
| | Wanateknolojia na Fundi wa Usaidizi wa Wataalamu wa Afya |
| | Wauguzi wenye Leseni wa Tabaka la Chini na la Juu |
| | Washauri wa Maumbile |
| | Wataalamu wa Radiotherapi |
| | Wataalamu wa Visaidizi vya Kusikia |
| | Wasaidizi wa Afya ya Nyumbani |
| | Wasaidizi wa Hospitali ya Wagonjwa Mahututi |
| | Wataalamu wa Viungo Bandia |
| | Wasaidizi wa Kimatibabu |
| | Waandaaji wa Vifaa vya Tiba |
| | Waandishi wa Matibabu |
| | Wasaidizi wa Duka la Dawa |
| | Wauguzi wanaotoa Damu kwenye Mshipa |
| | Wauguzi wa Nusukaputi |
| | Wakunga |
| | Wauguzi Watendaji |
| | Wauguzu Wasaidizi, Wadumisha Usafi, na Wasaidizi wa Wagonjwa wa Kiakili |
| | Wafamasia |
| | Wasaidizi wa Daktari |
| | Madaktari |
| | Wauguzi Waliosajiliwa |
| | Madaktari wa Upasuaji |
| | Matabibu |
| **Wafanyakazi wa Mstari wa Mbele Wasio wa Kliniki-** Wanaokaribiana na wagonjwa moja kwa moja wako katika **hatari kubwa** | Makasisi |
| | Washauri |
| | Wasaidizi wa Huduma ya Kibinafsi |
| | Mameneja na Wafanyakazi wa Jumuiya na Huduma ya Jamii |

| | |
|---|---|
| | Madereva wa Magari ya Abiria |
| | Wafanyakazi wa Huduma ya Mazingira |
| | Walinzi |
| **Wengine (wa kliniki) –** Wanaokaribiana kwa kiasi fulani na wagonjwa moja kwa moja wako katika **<u>hatari ya wastani</u>** | Matabibu wa Vitobo |
| | Matabibu wa Usikivu |
| | Matabibu wa Maungo |
| | Wanateknolojia na Mafundi wa Maabara ya Kliniki |
| | Mafundi wa Maabara ya Meno na Macho na Mafundi wa Vifaa vya Matibabu |
| | Wanateknolojia na Mafundi Wanaohusiana na Uchunguzi |
| | Wataalamu wa Chakula na Lishe |
| | Matabibu wa Kukanda Mwili |
| | Wataalamu na Mafundi wa Usalama Kazini |
| | Matabibu wa Mambo ya Kazi na Wasaidizi |
| | Daktari wa Macho, Wapeanaji |
| | Wachunguzi wa Macho |
| | Matabibu wa Kimwili na Wasaidizi |
| | Matabibu wa Miguu |
| | Wanasaikolojia |
| | Wahudumu wa Jamii |
| | Vinyozi, Wasusi, Watengeneza Nywelena Wanavipodozi |
| **Chakula/Rejareja–** Wanaokaribiana kwa kiasi fulani na wagonjwa moja kwa moja wako katika**<u>hatari ya wastani</u>** | Wafanyakazi Wanaopeleka Chakula |
| **Chakula/Rejareja-** Wasiokaribiana na wagonjwa moja kwa mojawako katika**<u>hatari ndogo</u>** | Makeshia |
| | Wapishi/Mameneja wa Kuandaa Chakula na Wafanyakazi |
| | Waosha Vyombo |
| | Meneja na Wafanyakazi wa Chumba cha Kulia na Mkahawa |
| | Mameneja wa Huduma ya Chakula |
| | Wafanyakazi Wanaohusiana na Maandalizi Mengine ya Chakula na Upakuaji |
| **Wengine wasio wa kliniki -** Wasiokaribiana na wagonjwa wako katika**<u>hatari ndogo</u>** | Wanasayansi wa Kibiolojia na Mafundi |
| | Wafanyakazi wa Huduma ya Watoto |
| | Matarishi na Wajumbe |
| | Watumaji |
| | Dereva/Wafanyakazi wa Mauzo na Madereva wa Malori |
| | Wafanyakazi wa Matengenezo ya Viwanja |
| | Waratibu wa Mafundisho |
| | Wafanyakazi wa Kufua na Dobi |
| | Mawakili na wafanyakazi wengine wa sheria |
| | Wakutubi na Wataalamu wa Ukusanyaji wa Vyombo vya Habari |
| | Makarani na Waendeshaji wa Mashine ya Barua |

| | |
|---|---|
| | Wafanyakazi wa Matengenezo na Ukarabati, Jumla |
| | Wanasayansi wa Matibabu |
| | Wafanyakazi wa Utekelezaji wa Maegesho |
| | Waendeshaji wa Swichibodi, pamoja na Huduma ya Kupokea Simu |
| **Huduma za utawala, ukarani na kifedha -** Wasiokaribiana na wagonjwa wako katika**<u>hatari ndogo</u>** | Huduma za Utawala na Wasimamizi wa Vituo na Wafanyakazi |
| | Mameneja na Wafanyakazi wa Uhasibu, Uwekaji Hesabu na Ukaguzi |
| | Mameneja na Wafanyakazi wa Wanunuzi na Ununuzi |
| | Watendaji Wakuu |
| | Mameneja na Wafanyakazi wa Fidia na Faida |
| | Wawakilishi wa Huduma kwa Wateja |
| | Wahojaji wa Ustahiki, Mipango ya Serikali |
| | Mameneja na Wafanyakazi wa Fedha |
| | Mameneja na Wafanyakazi wa Ofisi na Usaidizi wa Utawala |
| | Wachangisha Fedha |
| | Mameneja na Wafanyakazi wa Rasilimali Watu |
| | Mameneja na Wafanyakazi wa Mauzo |
| | Mameneja wa Huduma za Matibabu na Afya |
| | Wataalamu wa Kumbukumbu za Matibabu, Wanateknolojia na Mafundi wa Afya |
| | Wapangaji wa Mikutano, Kongamano na Hafla |
| | Mameneja wa Nyumba, Ununuzi wa Nyumba na Ushirika wa Jamii |
| | Mameneja na Wafanyakazi wa Mahusiano ya Umma |
| | Wataalamu wa Mahusiano ya Umma |
| | Wapokea-wageni na Makarani wa Habari |
| | Makatibu na Wasaidizi wa Utawala |
| | Makarani wa Usafirishaji, Upokeaji na Hesabu |
| | Mameneja wa Huduma za Jamii |
| | Mameneja na Wafanyakazi wa Mafunzo na Maendeleo |
| | Mameneja wa Usafiri, Uhifadhi na Usambazaji |
| **Kompyuta/Teknolojia ya Habari -** Wasiokaribiana na wagonjwa wako katika**<u>hatari ndogo</u>** | Mameneja na Wafanyakazi wa Kompyuta, Mifumo ya Habari na Hifadhidata |
| | Wataalamu wa Usaidizi wa Kompyuta |
| | Wafanyakazi wa Uingizaji Data na Usindikaji Habari |
| | Wataalam wa Teknolojia ya Habari ya Afya, Wasajili wa Matibabu, Wasaidizi wa Upasuaji, na Watendaji wa Huduma ya Afya na Wafanyikazi wa Ufundi, wengine wote |

## KIAMBATISHO CHA B: Kuamua Ikiwa Wahudumu wa Afya na Waitikiaji wa Kwanza wako katika Awamu ya 1a

**Algorithimu ya Kuamua ikiwa Wafanyakazi katika Mipangilio ya Huduma ya Afya* na Waitikiaji wa Kwanza wako katika Awamu ya 1a**




*Mipangilio ya huduma ya afya: Hizi ni pamoja na lakini sio tu hospitali za dharura na za urekebishaji; kliniki za wagonjwa wa kutembea na za huduma za haraka; vituo vya dialisisi; vituo vya kuchangia damu, viungo, na tishu; nyumba za uuguzi; huduma ya nyumbani; ofisi za wauguzi wa shule na mipangilio mingine (tazama Jedwali la 1).

**Mhudumu wa afya(na waitikiaji wa kwanza ambao huenda walikaribiana na wagonjwa kama ilivyofafanuliwa hapo juu): Wafanyakazi wanaolipwa au wasiolipwa katika mipangilio ya huduma ya afya ambao huwahudumia wagonjwa (yaani, daktari, muuguzi, n.k.) au wanafanya kazi katika maeneo ambayo wagonjwa wanapatikana (yaani, huduma za mazingira, makarani wa vitengo). Kikundi hiki kitajumuisha majukumu ya jadi ya huduma ya afya lakini pia kinaweza kujumuisha wengine ambao wamepata mafunzo rasmi ya matibabu ambayo huwawezesha kufanya taratibu za utunzaji wa kliniki. Kwa mfano, wataalamu wa masomo ya shule wasiokuwa na leseni hawajumuishwi mara kwa mara ndani ya ufafanuzi huu wa wahudumu wa afya isipokuwa ikiwa wamepata mafunzo kama haya. Mtu huyo hahitaji kuwa amepata digrii ya kliniki, lakini anatarajiwa kuwa anaendelea kukribianana wagonjwa wakati wa kazi yake, pamoja na wale wanaosambaza au kupeana chanjo ya COVID-19 kama wafamasia, wafanyakazi wa uchangiaji wa plasma na damu, wauguzi wa afya ya umma, wanamaabara wa COVID-19, na wasimamizi wa mazishi, wahudumu wa vyumba vya kuhifadhia maiti na wataalamu wengine wa huduma ya kifo.